

Kipindi Cha Mpito Jumuishi

Kipindi cha mpito katika muktadha wa elimu kina maana ya mpito kutoka ngazi/hatua moja hadi nyengine kama vile kutoka darasa au shule moja kwenda nyengine. Hiki chaweza kuwa ni kipindi kigumu- kwa wanafunzi, wazazi/walezi/ familia na walimu wao. Wanafunzi wengi huacha shule katika kipindi hiki au baada yake, hasa ikiwa wanafunzi hao watakuwa na mahitaji maalum ambayo hayatazingatiwa wakati wa mchakato huo.

Jee, ni changamoto gani wanafunzi hukumbana nazo wakati wa kipindi cha mpito?

Siwezi kufika katika mazingira ya shule yangu mpya wala kuzifikia sehemu mbali mbali ndani ya shule hiyo.

Sikuwahi kuyaona mazingira ya ndani ya shule yangu mpya hadi siku ya kwanza ya muhula. Nilikuwa na hofu.

Kila mmoja huona kuwa mimi ni 'mkubwa' na hivyo ni lazima niweze kukabiliana na mazingira ya shuleni. Bado nina hofu na nimechanganyikiwa!

Ninapata shida ya kuonekana fedhuli (sina heshima) kwa mwalimu wangu mpya kwa sababu siwezi kufahamu anachotaka nifanye.

Walimu wa shule yangu ya zamani walikuwa wakipanga jinsi ya kunisaidia katika masomo fulani. Shule yangu mpya haielewi kuhusu jambo hili. Mipango yote ya kunisaidia inabidi kuanza upya. Natamani mwalimu wangu wa zamani angeliendelea kushirikishwa.

Nina wasiwasi kuwa sitoweza kupata marafiki wapya wala kushiriki katika matukio mbali mbali shuleni.

Wazazi wangu hawashirikishwi sana hapa shuleni, sasa hivi nipo darasa la juu zaidi lakini bado ningependa waendeleo kuzungumza na walimu wangu ninapokuwa na matatizo/shida.

Hii ratiba ya shule yangu mpya inanichanganya. Sijui ninatakiwa kwenda wapi na saa ngapi? Kila mara huambiwa kuwa nimefanya makosa kwa kuchelewa kufika darasani.

Shule ipo katika eneo jengine tofauti. Nina hofu! Inatia hofu! darasani.

Ni vigumu kufaulu kwenda katika hatua/ngazi nyengine. Mitihani haijazingatia mahitaji yangu.

Sijazoea kuwa mbali na wazazi wangu kwa siku nzima.

Walimu wa shule hii wako tofauti na wale wa shule yangu ya zamani. Mbinu/Njia zao za ufundishaji ni tofauti. Siwezi kuzoea matarajio yao.



Vipi tunaweza kukifanya kipindi cha mpito kuwa jumuishi na chenye msaada zaidi?

Shule za maandalizi, msingi na sekondari, vyuo vya mafunzo ya amali/ufundi pamoja na vyuo vikuu vinapaswa/ni lazima kuwa na mipango/matamko ya kuwasaidia wanafunzi kabla, wakati na baada ya kipindi cha mpito.

Kuwe na wale wanaoratibu kipindi cha mpito kuelekea darasa au shule nyengine

Kuanzisha utaratibu/mfumo ambao walimu na wataalamu maalum shuleni wataweza kupeana taarifa na wenzao waliokuwepo kabla, au watakaokuja baada yao.

Kuhakikisha kwamba Mipango Binafsi ya Elimu inaekewa kumbukumbu vizuri na kupewa mwalimu/ shule mpya ya mwanafunzi anayehusika.

Toa mafunzo kwa wafanyakazi wote juu ya mahitaji ya kihisia, kimwili, na kitaaluma ya wanafunzi wanapohamia au kuhama shule na pia toa vifaa vya mwongozo.

Wape wazazi vipeperushi vinavyoelezea ni mambo gani ya kutarajia, na ni jinsi gani wao pamoja na shule wanaweza kuwasaidia wanafunzi katika kipindi hicho cha mpito ili kiwe rahisi kwao.

Wasaidie wanafunzi kuweza kutembelea darasa au shule yao mpya ili waweze kuzoea mazingira, watu na taratibu katika mazingira hayo mapya kabla ya kuhamia huko.

Wawezeshe walimu kuwatembelea baadhi ya wanafunzi majumbani kwao ili waweze kutambua mahitaji yao, familia zao na mfumo saidizi wa jamii.

Washirikishe wazazi/walezi katika kuandaa/kutayarisha mipango ya kipindi cha mpito.

Tathmini na rekebisha mitihani ya kuingilia au kumaliza shule pamoja na taratibu nyengine za udahili. Rekebisha taratibu hizo ziwe bora na zenye manufaa pia kwa wanafunzi wenye ulemavu.

Hakikisha kwamba shule za sekondari zina taarifa sahihi kuhusu vyuo vya elimu ya amali/ufundi na vyuo vingine vya elimu ya juu ambavyo ni jumuishi na vinaweza kufikiwa na watu wenye ulemavu.

Hakikisha kuwa shule za sekondari, vyuo vya elimu ya amali/ufundi na vyuo vyengine vya elimu ya juu vinatoa huduma za mwongozo wa ajira zilizo sahihi na zenye kuwapa ushauri na kuwashajiisha/kuwahamasisha wanafunzi wenye ulemavu.